

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

VERBATIM REPORT OF

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,

EMUHAYA CONSTITUENCY,

KIMA MISSION CHURCH

Wednesday, August 7th, 2002

CONSTITUENCY PUBLIC HEARING- EMUHAYA CONSTITUENCY, ON
WEDNESDAY, JULY 11TH, 2002 AT KIMA MISSION CHURCH

Present:

Com. Pastor Zablon Ayonga
Com. Dr. Abdirizak Nunow
Com. Mutakha Kangu

Secretariat Staff in Attendance:

Samuel Wanjohi - Programme officer
Hellen Namisi - Assistant Programme Officer
Grace Gitu - Verbatim Recorder
Agnes Auma - District Cordinator

Meeting started at 10.00am with Com. Pastor Ayonga in the chair.

Mrs. Doris Orison: Asubuhi ya leo tuna bahati kuwa na wageni wetu ambao ni Commissioners na tunawakaribisha nyinyi nyote pamoja na hao, mujisikie muko nyumbani. Na kabla hatujaanza mkutano wetu, tutauliza muhubiri atuweke kwa maombi kabla tuendelee mbele. Na karibisha muhubiri wetu, Reverend Wycliffe Otundo. Kuja uombe.

Rev. Wycliffe Otundo: Tujiweke katika utukufu wa Mungu.

Prayer: Tumekaribia hapa katika kanisa lako takatifu kusudi tusikizane katika maisha yetu kwa kudumu katika ulimwengu ulio na mashaka mengi. Watumishi wako wamefika hapa, wakitafuta maisha ya wenzio na maisha ya dunia yetu na maisha ya Kenya yetu na utawala wetu. Bwana utupe mawazo mazuri. Uwape akili leo, uzungumze na wao katika mawazo yao, jinsi wawezavyo kutawala Kenya yetu ilio na mashaka mengi na adui wengi na watu kutosikizana, Bwana tunakuomba zunguka katika mioyo ya watu wako katika Kenya, washikamane katika kusema, washikamane katika kuongea, kufanya kazi pamoja, kujua wao ni watu wa Kenya. bwana bariki hawa wazee, bariki vijana tulionao, bariki Kenya yetu, Bwana ututawale. Ingawa tunataka mtawala, zaidi sana tunataka mtawala kutoka kwa uwezo wako. Bwana bariki hawa wageni, na neno watakalo zungumza,

Bwana liwe na chumvi, liwe la msaada la kusaidia watumishi wako Wakenya. Bariki Kenya yetu kwa jina la Yesu Mkombozi wetu, Amen.

Mrs Doris Orison: Tumefika wakati wa kujuana. Lakini kabla tufanye hivyo, ningependa kumpatia muhubiri ambaye ni msaidizi wa yule anasimamia kanisa hili, atuingize sisi kama wageni wake ili tujuane, karibu muhubiri.

Rev. Patrick Maina: The Commissioners, your pannelists, and all in attendance, my names are Reverend Patrick Maina, standing here on behalf of the Bishop of the Church of God in East Africa, the Right Reverend, Dr. Byron Makokha. We are most delighted to host you here as we participate in this most noble occassion of collecting views. Ni madhumuni yetu ya kwamba munapointia hapa siku ya leo, ijapokuwa tuko katika hekalu, lakini mujisikie uhuru kiasi cha kutoa maoni yenu na mazungumzo yenu katika mjadala wa leo kwa uhuru wote lakini tukijua ya kwamba, vile muombaji amesema, Mungu ndiye mkuu wetu sote. Lakini tuwe uhuru kama Wanakenya, mujisikie uhuru katika jengo hili kuchangia makusudio ya lengo la leo. Na tunawakaribisha kwa moyo wote. Mujisikie muko nyumbani. Tuko sehemu moja na nyinyi, hata kama ni kanisa, lakini we are still part of the Kenyan society. You are most welcome. Thank you.

Mrs. Doris Orison: Baada ya kukaribishwa, ningependa kuwajulisha ya kwamba, Emuhaya constituency imekuwa ikisimamiwa ama ikiongozwa na kamati teule ya Constituency Constitution Committee, na imekuwa ikiongozwa na Mrs Obuluta, who has just arrived. Na mimi nikiwa secretary wa kamati hiyo, ningetaka kumuingiza ili atujulishe kamati ya constituency na ningependa pia kuwajulisha kwamba tuna mikutano miwili katika division hii. Huko Eburnangwe, kuna kikao katika Itile church, Eburnangwe, na wale ambao wanatoka sehemu ile tumewaambia waende watoe maoni yao huko chini Eburnangwe na Members wa kamati wengine wameenda huko. Kwa hivyo hapa tuna wana kamati watano na pia Bishop Reverend Makokha ni member wa kamati hii na ametuambia kwa sababu ana kazi zingine, sisi tutaendelea. Kwa hivyo namuingiza Madam Obuluta, ajulishe kamati yake kwa Commissioners na nyinyi wote ili tuanze. Karibu Madam Chairman.

Mrs. Getrude Obuluta: Commissioners na wageni wetu, hamjambo?

Response: Hatujambo.

Mrs. Getrude Obuluta: Niko na furaha kuwakaribisha hapa kwetu. Na hawa ndio wana kamati wale tumekuwa tukifanya kazi nao. Tukianza na George Oredo. Yeye yuko kutoka Wehomo location. Halafu tuko na Arthur Etale, kutoka Central Bunyore. Halafu tuko na Dorah Orison, kutoka East Bunyore. Halafu tuko na Christopher, yeye alikuwa representative wa disabled. Sasa ningependa kuwakaribisha Commissioners, waendeleo na kazi yao. Asanteni. Mimi mwenyewe naitwa Getrude Obuluta kutoka West Bunyore.

Com. Pastor Ayonga: Mrembe mwesi. Mimi ni Mnyore, ni Mnyore, lakini naishi upande wa Kisii ingawa kuna Mnyore

mwingine hapa ambaye si Mnyore haswa lakini anazidi kunipinga, anataka nisifuute roots. Unajua watu wenu ni watu wenu, upende usipende. Kama tungeita mtu leo aje achukue damu ya Wanyore, yangu itapatikana huko tu. Asubuhi ya leo, tumefurahi sisi kama wawakalishi wa Commission yetu ya kuchukua maoni kuwa hapa kwenu. Na kwa maana ni lazima tuanze mapema na tufuate taratibu, kwanza nitawauliza Commissioners wawasalimu. Lakini kabla hawajawasalimu, upande ule, tuna secretariat, watu ambao wanatusaidia katika kazi hii kwa kuchukua record, kwa kuchukua memorandum ambazo mumetuma, kwa kunasa maneno yenu, kwa kuandika maneno yenu.

Ningalipenda ndugu Wanjohi usimame. Kila wakati ukishamaliza maneno yako hapa mbele tutakwambia uende kule. Yule atakuandikisha, uweke kidole, utoe memorandum yako kule kwake na yeye ataiweka. Halafu tuna dada wawili hapa. Mmoja anachuka maneno yenu yakinaswa katika kanda. Hebu waonyeshe hiyo kanda. Huyu ndiye Grace, yeye, wakati mwingine mutakuja kuona hapa huyo mtoto wa Wanyore haandiki na utanza kufikiri amedharau maneno yangu au utamwona daktari hapa haandiki au mimi. Nasema mimi nilipokuwa nikisema sikuona wale watu wakiandika. Maandishi yetu hapa ni ya kuchukua pointi fulani ambazo pengine tunataka kukuliza maswali.

Lakini kule, kila neno utakalosema litashikwa. Kwa hiyo kazi yetu, misemo yenu yote itaingia hapa kwa kanda. Halafu baada ya Grace tuna dada mwingine. Helen ambaye atakuwa pia anaandika na kutunza record ya mambo yote jinsi yanavyoendelea. Kwa hivyo hao dada Grace, Hellen wana kazi. Wanjohi ana kazi na sisi hapa tuna kazi ya kuwaelekeza.

Lakini sasa kabla hatujaanza nataka mupate salamu ambazo ni za pekee kutoka kwa Dr. Abdirizak Nunow. Huyu ndiye anatoka mbali kuliko sisi sote. Si mimi nilisema mimi ni Mnyore, mimi nilisema “mrembe” na hebu nikwambie kule tunaposema kile kinyore chenyewe, tunasema “Omurembe mwesi”, unasikia. Si kwamba nina-guess, ni omurembe mwesi, mwesi ni wote, na omurembe ni amani. Hiyo ndiyo original na tulienda nayo huko tulipowaacha hapa. Mulichoka, milima pia iko mingi, mawe ni mengi, basi mukaona mukalie hapa na hakuna ubaya. Ndugu yako ni ndugu yako hata awe wapi. Kwa hiyo mtasalimiwa salamu ambazo zimetoka mbali, kule North Eastern na amezibeba, wakati mwingine alitembea nazo na miguu, wakati mwingine alizibeba akiwa juu ya ngamia, wakati mwingine amezibeba akiwa kwa ndege, wakati mwingine amezibeba akiwa kwa motokaa, na hizo si ni salamunzito?. Daktari salimia watu.

Com. Nunow: Asante sana Commissioner Ayonga. Mimi vile muliambiwa kwa majina ninaitwa Abdirizak Nunow, mmoja wa Commissioners wa Tume. Wananchi wa Emuhaya constituency, nina furaha sana kuwa nanyi leo, na natumaini kwamba mutatoa maoni yenu bila hofu, bila kuogopa kitu chochote, na jinsi mpendavyo. Kusudi ni kwamba lile liko chini zaidi kwenye bongo la mtu litoke, liweze kusaidia kutengeneza Kenya mpya. Karibuni na asanteni. Ahsalamu aleikum!

Com. Ayonga: Mumesikia hizo salamu ni tofauti sana? Eeh, mulisema aleikhum salamu. Vizuri sana. Mimi ni Pastor Zablon Ayonga, Commissioner, na leo nitakuwa kama mwenyekiti kwa wakati wa asubuhi, lakini sasa wacha huyu mtoto wetu wa kando hapa, awasalimie na tena awaambie taratibu. Taratibu tutafanya mambo haya namna gani. Salimia watu kwa Kikisii sasa.

Com. Mutakha Kangu: Asante Bwana Pastor Ayonga.

(Kiluhya dialect) Mimi naitwa Mutakha Kangu, nimekuwa hapa siku ingine tukizungumza na nyinyi, na nikamwambia

(Kiluhya dialect). When I am teasing him as a grandfather from whom I get wisdom, I normally tell him that the Kisiis' were looking for baridi, wakatuacha hapa wakasonga huko mbele, halafu wamefika huko wameharibu kiluhya. Badala ya kusema 'makuru', wanasema 'makoro'.
(?) Wanasema

(?) si ni kiluhya tu wameharibu kidogo? Sasa n dio unasikia yeye akisema yeye ni Mnyore kwa sababu nimemwambia they are not Kisiis', they are luhyas who have just spoilt Kiluhya. Asante sana. Sasa, siku ya leo ni siku yenu ya kutoa moni kwa Tume ya Kurekebisha Katiba na kama hatujaanza, tuna utaratibu tunaeleza, ndio watu waweze kujua vile mkutano unaendeshwa.

Jambo la kwanza ni kwamba huu ni mkutano wa Tume ya Kurekebisha Katiba. Kiongozi wa kanisa ametukaribisha na tuko na yeye, na munaona yeye mbele yenu. Mkutano wa leo si wake ni wa kurekebisha Katiba na hata kama mkiangalia kati yenu, pengine kuna viongozi wa serikali, provincial administration, pengine ma-chief, sub-chiefs, tunasema huu ni mkutano wa Tume na kwa hivyo hata kama hao watu wa serikali wako katikati yenu, wasiwe ni watu wa kufanya wewe uwe na uoga usiseme yale unataka kusema. Tumefanya kazi na watu wa serikali ikakubalika kwamba mradi wa kurekebisha Katiba, ni mradi wa Wakenya wote, ni mradi wa serikali, na kwa hivyo watu wa provincial administration wamekuwa wakisaidiana na sisi, wanasaidia committees zetu on the ground na wamekuja hapa wakijua, hata nao wamekuja kutoa maoni yao, sio kuja kutisha wewe usitoe maoni.

Kwa hivyo ujisikie uhuru. Feel very free to state your views, kwa sababu tulisema kuna shida hapa Kenya kulingana na vile tunaendesha maneno yetu, na tukaamua tutafute ni shida aina gani na tutafute suluhisho itakuwa nini na hatuwezi kufanya hivyo ikiwa wewe utakuja hapa na tena uogope kusema yale uko nayo. Hata kama unataka kusema provincial administration hatutaki, feel free to say that because those are your views. Hata kama unataka kusema, " ooh, makanisa yamekuwa mengi sana, don't fear because mtu wa kanisa ako hapa. Juzi tumekuwa huko Teso na mwingine akatuambia, we seem to be investing too much in churches when people are going hungry. We need to kuchunguza haya maneno. So even if you wanted kusema hivyo, hapana ogopa kwamba kiongozi wa kanisa ako hapa mbele kwa sababu tunatafuta suluhisho ya shida ile tuko nayo. We must be able to put all our ideas together ndio tujue tutaelekea upande gani. Hata kama mwenzetu ni Pastor na unataka kumwambia," ooh, haya maneno ya kanisa hatutaki, wewe mwambie tu. Hapa leo ni Commissioner tu, yeye hapana Pastor. Hatahubiri leo. So, zungumza ukiwa free.

Jambo la pili, maoni tunataka kuchukua kwa kutoka kila mtu, wazee, wamama, vijana, walemavu na watu wa aina yote. All the diversities zenye muko nazo hapa. Tunataka mchanganyiko wa watu wote na wakati mtu anazungumza tunasema tunataka tuwe na uvumilivu. Usisikie mtu anasema mambo hukubaliani nayo, uanze kupiga kelele. Mpatie nafasi aseme yake, amalize na wakati

na wewe utapatiwa nafasi utaweza kusema lile hukubaliani na yeye na yale unafikiria inafaa badala ya yale yule mwingine amesema. Tukifanya hivyo, tutaenda sawasawa. Sababu ingine nasema tusipige kelele, ni kwamba mumelezwa maneno munayosema tunaandika, na tena tunanasa kwa mtambo wa kunasa sauti. Na mukianza kupiga kelele, hiyo ita-interfere na ile process ya kunasa maneno. Baadaye tukikaa tukitaka kusikiza maneno yaliyotoka Kima tunapata tulirudi na kelele badala ya maneno. Kwa hivyo, muwe watulivu na hapo tunasema hata ikiwa mtu ansema jambo linalokufurahisha, hapana anza kupiga makofi, you will interfere with the recording. Tulia akimaliza

(in luhya dialect)

Translation: Umpatie sifa huko nje, badala ya kupiga makofi hapa. Utaharibu the record.

Maoni tunachukua kwa namna tatu. Ya kwanza ni watu wenye wana maandishi, lakini hawataki kuzungumza lingine lolote. Yake ni kuleta maandishi yake hataki kuelezea hayo maandishi, hataki kuzungumza lolote. Ukiwa wewe una maoni aina hiyo, unaweza toka pole pole unapeane pale, jina lako linaingizwa kwa register, unaweka sahihi, na details zingine utaulizwa zitawekwa. Na ukitaka kukaa usikize wengine wanazungumza nini, unakaa. Ukiwa na shughuli mahali pengine unataka kwenda, unaweza toka pole halafu uende, utakuwa umepeana maoni yako.

Namna ya pili, ni wale wana maandishi, na tena wanataka kuelezea hayo maandishi. Unataka kuzungumza juu ya hayo maandishi, unataka ku-explain. Tutakupa nafasi ukae hapa ueleze, lakini tunasema isiwe nafasi ya kukuja na wewe unataka kusoma yote umeandika. Kwa sababu saa ingine itakuwa mrefu, inachukua muda mrefu. Jaribu kumulika tu yale ya muhimu. Highlight the key issues kwa sababu utatupatia, tutaenda kusoma yote yenye umeandika. Utafanya hivyo na ukimaliza upeane pale jina lako liandikwe uweke sahihi.

Namna ya mwisho ni wale hawana maandishi yoyote, lakini wana mambo wanataka kutueleza kwa mdomo. Tutakupatia nafasi ukae hapa ueleze tunaandika na tunanasa na ile mitambo ya sauti. Hata na wewe ukimaliza uende uandikishe jina uweke sahihi. Huo ndiuo utaratibu tunafuata. Kwa wale wana maandishi na wanataka kuelezea hayo maandishi, tunasema tutakupatia dakika tano ya kueleza hayo maandishi. Kwa wale hawana maandishi, tunasema tutakupatia dakika kumi ya kujieleza. Sababu ni kwamba yule hana maandishi, hana kitu kingine atatuachia, na kwa hivyo ni afadhali tumpatie muda aeleze mambo yake yote tuende nayo. Wale wana maandishi, tutaweza kusoma maandishi baadaye, but tuna discretion, wakati tunaanza mkutano watu hawajakuwa wengi tunaweza kukuongezea wewe muda kidogo.

Wakati inaanza kufika jioni watu ni wengi na masaa inaenda tunaweza kupunguza hata hiyo masaa. Sasa tuseme badala ya dakika tano ni dakika tatu na wewe ujaribu kutusaidia ndio tuweze kusikiza watu wengi. Pia tuna discretion tunasema kuna watu tunaweza angalia, tunaweza kusema huyu ni opinion leader, na ako na maneno ya wengi afadhali tumwongeze muda kidogo aeleze mambo yake kwa niaba ya wengine. Ama tukianza kufika afternoon, wengi wenu mtapata yale mlikuwa mnataka kuzungumza yameshatajwa na wengine na kwa sababu muda inaenda tunasema, saa ingine hakuna haja kurudia yote. Unaweza guza pale na pale, halafu ulete ile ingine haijazungumzwa na mtu mwingine. Ama kama uko na a new perspective kwa ile

imezungumzwa, na wewe utupatie that new perspective ndio tuweze kupata mambo yote. Hivyo tutasikiza wengi na tupate maneno mingi.

Kwa hivyo tuweze kupata huo utaratibu na tuende sawa sawa. Ukimaliza kuzungumza tunaweza kuwa na maswali ya kukuuliza wewe kufafanua mambo umesema. Tutakupatia hayo maswali, unatujibu kama una majibu. Kama haujafikiria, hauna majibu, tena si lazima ujibu. Unatuambia hukuwa umefikiria, pengine utaenda kufikiria baadaye. So muweze kuelewa.

Na mwisho, lugha, tunasema hatutaki kuambia watu kuja mbele yetu uzungumze lugha fulani. Wakenya tulisema watoe maoni yao na kwa hivyo hatuwezi kupeana nafasi na tena tuinyang'anye kwa kusema lazima utumie lugha fulani. Uko na uhuru wa kuchagua mwenyewe ni lugha gani utatumia itakuwezesha kueleza mambo yako bila shida. Ukitaka kuzungumza kiingereza uko na uhuru. Ukitaka kuzungumza Kiswahili uko na uhuru.

(Kiluhya dialect) (?)

Halafu tutatafuta hapa mtu wa kutafsiri kwa wale hawaelewi, waelewe unasema nini lakini (?)

(Kinyore dilect)

Feel free say everything you have to say kwa sababu saa hii tunatengeneza historia ya inchi hii na baadaye itakuja kujulikana. Saa hii tukifanya watu wanaweza kufikiria ni mambo ya mchezo but much later watu watakuwa wanasoma wanaona kweli hawa watu walikuwa wanafikiria nini na nini. Juzi nilikuwa ninasoma ile inaitwa the Federalist Papers zile ziliandikwa na wale walitengeneza Katiba ya Amerika over two hundred years ago. Na ukisoma unaona kweli walikuwa wamefikiria mambo mengi. So yale tunasema hapa leo, we will preserve it for many years to come.

(Kiluhya dialect)

Com. Ayonga: Sasa nasikia anawaambia mtaongea kwa Kinyore lakini sijui kwa nini hakusema pia mnaweza kuongea kwa Kikiisi kwa maana hiyo yote ni mang'ana ee na hiyo kuboranga yote zote tunabora. Kwa hiyo ikiwa mtu atashindwa kuongea Kinyore aongee Kikisii na tutamsaidia tutakuwa na wale wanaotafsiri. Sasa asante Commissioner Kangu kwa maelezo ambayo umetupa. Kuna kitu ambacho tutafanya, tutafuata orodha ya karatasi ambayo mlioji-register mlipo toka kule nje. Na tutajaribu sana kuifuata lakini wakati mwingine tunaweza pia kuwacha kuifuata na tukafuata mambo tofauti.

Tofauti hii inakuja namna hivi, ikiwa katika watu ambao wameingia mtu anaweza kuwa mgonjwa na yeye amekuja nyuma lakini amejisikia ana homa huyo mtu, tukijulishwa kupitia kwa program officer, kwa secretary hapa na kusema mimi ni mgonjwa, tutampa nafasi. Kwa hiyo hatutafuata list, tutamuuliza tu jina lake ni nani. Pia ikiwa kutakuweko mtu hapa ambaye ni mzee sana, mama mzee sana au mwanamume mzee sana na hatutaki kumweka katika hizi bench ngumu kwa muda mrefu, tunaweza kumpatia nafasi. Ingame, inaweza kuwa watoto wa shule. Mtoto wa shule akija hapa anataka kutoa maoni na tunajua huyu mtoto amewacha wengine wakisoma, tutampa nafasi aseme maneno yake, arudi darasani. Au mama mja mzito tutampa nafasi, au mtu mlemavu wa namna fulani ambayo tunaona kukaa kwake kwingi hapa kutamdhuru tutampa nafasi. Lakini zaidi tutajaribu

kufuata hii list jinsi ambavyo first come first served. Tume elewana? Kwa hiyo yeyote asije anung'unike kwamba kumbe naona uko upendeleo hapa, mbona naona yule ameitwa na yeye amekuja saa hii na mimi nimekaa hapa toka asubuhi.

Kitu kingine, tafadhali tutii time. Mnajua tukishirikiana kwa kutii mambo, yana-kuwa rahisi. Mara ingine mtu anakuja anazidi kurudia rudia kile ambacho anakisema na tukimwambia time yako imekwisha anasema ngoja kidogo, ngoja kidogo. Hata fikiria kwamba tutakuja hapa tukunyang'anye microphone, hatuwezi kufanya hivyo. Lakini tunataka ujue kwamba Wanyore wote ambao wako hapa wanataka kuongea. Na kwa hivyo hao they are as important as yourself. So hebu tutunze time.

Sasa ninaanza na kwa kuanza ninasema hiki kikao cha Constitutional Review Commission tumekifungua sasa kirasmi. Na tunaanza kazi ya Constitution Review na kazi hii jinsi ambavyo Commissioner Kangu alisema, hakuna kupiga mikono makofi hakuna. Tuko kama watu ambao tuko kotini na zaidi ya yote niwakumbushe kitu kingine, hapa tuko katika nyumba ya Mungu. Hii nyumba ni nyumba ya Mungu, ilijengwa kwa ajili yake. Kwa hivyo ingawa tutatoa maoni yetu, shida zetu, namna zote jinsi tunavyomletea Mungu wakati wa maombi, hebu pia tutoe heshima kwamba hatuko katika baraza hall tuko katika nyumba ya Mungu na ni yeye atakayetusaidia kutengeneza Constitution ambayo ni sawa. Kumbuka amri zake ni kumi nazo zimeguza kila sehemu ya amri yeyote ambayo inatengenezwa hapa ulimwenguni. Zake ni perfect na hazibadiliki.

Ninaanza sasa. Unapokuja hapa mbele kitu cha kwanza tunataka ufanye ni kusema majina yako, 'mimi ni fulani fulani.' Ikiwa unawakilisha kikundi unasema kikundi hicho. Lakini kama huwakilishi kikundi sema jina lako na utuambie maoni yako. Msiwe mkija hapa muanze kusema Bwana chairman, mkuu wa nini, hivi na hivi. Zile salamu nyingi nyingi. La! Hakuna hiyo. Tuko hapa katika serious business, kuja tu utuambie maoni yangu ni hivi na hivi na hivi. Na kama una memorandum na hutaki kuongea juu ya hiyo memorandum, hata saa hii wewe unaweza toka hapo usingoje kuitwa ukaenda hapa kwa Bwana Wanjohi na ukatoa memorandum yako ukajiandikisha na ukatoka ukaenda kufanya mambo yako. Hiyo pia, ruhusa hiyo iko. Usije ukakaa hapa kama mahabusu kwamba jina lako halijaitwa. Unaweza kuja na memorandum yako, submit it and register, leave for your other businesses. Sasa ninaanza. Bensewel Muchilwa.

Bensewel Muchilwa: Ma-Commissioners wetu na ma-cordinators na wananchi wote hamjambo? Hamjambo tena?

Com. Ayonga: Bwana Muchilwa hiyo ndio nilisema tusifanye, sikusema tufanye hiyo.

Bensewel Muchilwa: That is alright, we learn by mistakes. Okay my name is Bensewel Muchilwa. I'am a representative of Kenya National Chamber of Commerce and industry Vihiga District based in this division of Emuhaya. Now, I have a written Memorandum here which I am going to present. But before I present this memorandum, I have drawn a summary of the contents of the memorandum which I would like to read to the audience here to know what the bussines community of Emuhaya is talking about. The views that we have requested to make to the Commission, may be I'll request the Commissioners to bear with me because the summary is abit long but I'll try to shorten it as much as possible.

Now this is a summary of Constitution views of Emuhaya business community under the Kenya National chamber of Commerce and Industry Vihiga district.

We need a preamble in our Constitution. In the preamble, Kenya's vision of nationhood should be set out clearly as we Kenyan citizens. And the Kenyans should own the Constitution.

Directive principles of state policy. We need statements in our Constitution capturing a national philosophy and guiding principles. For example, all citizens must be equal before the law including the President.

Parliament must not be allowed to pass certain matters or issues without consulting with citizens of the country like the extension of life of Parliament, increment of salaries for Parliamentarians, civic leaders and civil servants in general.

We must have a Salary Commission which should be charged with the responsibility of reviewing salaries and other remunerations for all other public servants at large.

It must not be mandatory that presidential candidates be elected Member of Parliament but be nominated by his or her party and subject to having attained the minimum age of thirty-five years or above and a required percentage of votes. That is 33.3% or a third of the total votes in the eight provinces of Kenya. If an elected Member of Parliament is appointed minister, he or she should relinquish the constituency seat and people allowed to elect another representative.

Constitutional Supremacy. (?) practise whereby Parliament has been allowed to change any part of the Constitution by a majority vote of 65% is unfair and must cease. But should amendments be necessary, Parliament should be allowed to draft the same and refer them to the public through referendum by Special Commission to be appointed.

For citizenship, anybody born in Kenya, I mean anybody born in or outside Kenya but whose parents are both Kenyans by birth will automatically become Kenya citizens. Foreigners who want to become citizens of Kenya shall have to be of good reputation with tangible assets or investments in Kenya and must surrender any other citizenship.

Foreigners who marry Kenyans and reside in Kenya, their children can only become Kenyan citizens by naturalisation if the father is a foreigner. And if the father is a Kenyan by birth, then they automatically become Kenyan citizens. The Constitution of Kenya should not allow dual citizenships. Kenyan citizens should be identified by national identity card, birth certificate and Kenyan passport.

On defence and national security, the disciplined forces must be established by the Constitution. Security council to be established by the Constitution to take charge and responsibility of disciplining Armed Forces, advising the executive on security measures before declaring war under Parliament's guidance.

Political parties. The Constitution should restrict political parties to three only at a time and should regulate the formation and management of the same. The parties should not only be for political mobilisation but also involve themselves in the development projects, checking and balancing the ruling party through Parliament. The government of Kenya should finance all political parties during elections.

Now, structures and systems of government...

Com. Ayonga: Hebu nikumbushe. Nataka ujue haya maandishi sisi tunaenda kusoma...(naudible)

Anza kuona ni point gani utakuja utuambie infact you should not come here to read for us tutaenda kusoma na tuna computer huko mambo yetu yote yataingizwa. Hiyo maana yake nimesema ukiwa (?) una maelezo unaweza kutukabidhi hiyo memorandum. Nakupa dakika mbili tu umalizie, mmeelewa?

Bensewel Muchilwa: Okay vile Bwana Commissioner amezungumza hivyo si vibaya nitajaribu kuwacha mengine. Na nilikuwa nafikiri kwa sababu na-represent a whole constituency, wanabiashara wote kama wangukuja hapa wote...(Interjection) Okey. Now, being Members of the business community and main stake holders of the economy, we feel the government should have been very fair to its people. Instead of protecting these young business community and young , it has subjected them to very unfair competitions. Consequently, most of the indigeneous businesses which are unable to cope up are collapsing gradually and vanishing away. We feel in order to assist the young community grow, the purchase price for goods should be seriously looked into. By purchase price of every category of goods like manufacturers warehouses and whole salers should be informed in every budget. I'll go to another point.

Basic rights on succession and inheritance. The current Constitution and law provides for daughters to succeed and inherit their parents property along side with their brothers and other dependants. That is, things like pieces of land, premises and other properties owned by their parents. Consequently this practise discourages the daughters from getting married since they feel they can peacefully settle for life in the property given. Eventually they end up cohabiting with relatives and other Members of the clan thus incest and producing illegitimate children in disappointment and embarrassment of the clan and society in general.

In the African customs and traditions, a daughter is supposed to be married away from her parents home or clan to either a foreigner or a man distant from the clan in relationships. There, she is supposed and she can easily access her husband's property by succession or inheritance after the husband's death. The new Constitution should therefore rule out this practise and be entrenched with only sons as successors and inheritors of their parents properties or estates. Only daughters who may be permanently disabled or incapacitated and cannot marry may be accorded the same privileges as boys. There's a common attitude in one's children assuming the right to demand property or some privileges from their parents after or before death. This may be in order but the law remains silent as to whether the parent is also entitled to such demands from the son after he dies

leaving behind a young or childless widow who might abscond after selling away the deceased's property leaving her dependants miserable.

The new Constitution must therefore state clearly, that the parent is the rightful person entrusted with overall responsibility of the son's estate if the latter dies earlier. He will be key player in all matters relating to the distribution of the son's estate and property at all times. This practise is intended to secure a man's property against a deceitful wife who may wish to escape away with the property after the man's death. Thank you. (Interjection) Yes please.

Com. Ayonga: Asante sana. Sasa unaweza kuchukua hiyo memorandum kule, utaambiwa mambo ya kufanya. Unaacha hiyo hapo chini. Asante. Next ambaye tutamwita ni Ishmael Ombwara. Natumaini wale wote mlio na memorandum mmeanza na kuangalia na kuona main points ambazo mtasema. Ishmael sema majina yako na endelea.

Ishmael Ombwara: Majina yangu ni Ishmael Ombwara. Natoka Luanda division, hii constituency, Vihiga District. Na ningependa kuongea juu ya crime.

Crime ni kitu ambacho hakitatanishi serikali peke yake, kinatatanisha hata sisi wananchi. Na mambo mawili ambayo yanasababisha crime kwenda juu ni umaskini na ukosefu wa kazi. Na wale watu ambao wanasababisha crime kwenda juu ni watu kama chokora, watu ambao wameacha kazi either kwa majeshi ama kwa civilian jobs. Na jinsi ya kusaidia kupunguza crime... ama kwanza ni kusema kwamba serikali isifanye mzaha na hiki kitu kinaitwa crime. Kwa sababu ni time bomb. Crime na umaskini ni time bomb ambayo inaweza kuiangamiza nchi yoyote kwa wakati wowote. Kwa hivyo serikali isimame na ianze kuchukua hatua mathubuti juu ya crime. Na vile nimesema watu ambao wana sababisha crime ni watu kama chokora na watu ambao wameacha kazi either kwa majeshi ama civilian jobs. Na jinsi ya kusaidia hawa watu wasifanye crime kwenda juu, kwanza watu kama hawa chokora ningehimiza serikali iwajengee makao nje ya miji mikubwa. Outside the main towns wajengewe makao huko na walindwe hata kama ni kulindwa na askari, walindwe huko, walishwe huko na wasitoke huko.

Kwa sababu hawa chokora wanafanya mambo mabaya sana sehemu za town sehemu za miji. Wananyang'anya in broad day light hata saa zingine wana-rape na ikiwa ni hii mambo ya kuongeza ukimwi naweza kusema chokora wana-play a big part ya kuongeza ukimwi, juu kwa sababu ya raping na wanatisha watu na mavi, ambao wanawanyang'anya pesa wanawatisha na mavi. Sasa vitu kama hivi vinaletea nchi aibu. Na jinsi ya kukomesha hawa machokora nimesema ni kuwajengea makao nje ya miji mikubwa na walindwe huko. Walindwe wasitoke kwa hayo makao kurudi town tena. Na hao ni wale chokora ambao walizaliwa na Aids victims. Lakini kama ni chokora ambao wazazi wao wako hai, bado wako hai na wako able, basi hao wazazi wafuatwe na walazimishwe kuishi na hao watoto wao ama sivyo wapatiwe kifungo cha juu, kifungo kirefu ambacho kitakuwa funzo kwa wengine, kufanya watu wengine ambao wanazaa tu watoto carelessly na kuwatupa ovyo ovyo waogope.

Na hawa ex-servicemen, upande wa ex-service men, tuseme watu ambao walikuwa kwa majeshi kama ploisi, army ama GSU ambao walifutwa on disciplinary offences, ningepomba serikali ifikirie kitu cha kuwasaidia nacho. Ikiwa itawapatia loan ya kufanya biashara, ikiwa itawapatia kazi ya ki-civilian, kwa sababu walikuwa wakizoea pesa, wasijiingize kwa hizi gang groups ambazo

zina-terrorize wananchi. Serikali ifikirie jinsi ya kuwasaidia hawa ex-servicemen.

Mwisho ningeomba Kenya iwe welfare state kama America na ulaya ambapo watu ambao hawana kazi, tunaambiwa na vyombo vya habari ya kwamba kuna watu hapa Kenya ambao wanapata mishahara minono minono. Wengine nasikia hata wanapata milioni, milioni mbili, ngapi na hizo na resources zingine ambazo serikali inajipatia pesa, hizo pesa, badala ya watu wengine kupata mishahara minono, hizo pesa zingine zipunguzwe zipatiwe watu ambao hawana kazi wapate kitu kidogo kidogo ili nao wasifanye crime kwenda juu.

Com. Ayonga: You have made your point kwamba tuwe na welfare State. That is the most important thing. Cha mwisho?

Ishmael Ombwara: Ni hiyo tu.

Com. Ayonga: Asante Bwana Ishmael, unaweza kwenda kule ujiandikishe. Next tunaye J. Bukachi.

J. J Bukachi : The chairman of the session, I'll be very brief. Naitwa J J Bukachi ama Josphat Jaques Bukachi. I am going to comment on the kind of the state we propose.

We propose that we have a federal state comprising eight different states. This will help to bring the service to the people. Tukikuwa na state kama nane vile tunasema provinces kama North Eastern, Western... ziwe scrapped ili tuwe na Western state, Central State, Nairobi State, Eastern state and so on. In these States tuwe na governors ambao watapeleka servise kwa people and these governors wawe elected through a secret ballot. And the new Constitution to form an electoral college whereby the eight different governors from the eight states form an electoral college whereby one of them becomes the President, Executive President, a Prime Minister, a Deputy Prime Minister, and a Deputy President. When I talk about a Deputy President I mean a man who has authority just like the sitting President.

I propose ya kwamba important Institutions like the courts, a supreme court be introduced into the system. Things like the Central Bank, the Immigration department and the Attorney general, registrars office, all of these important institutions be decentralised from Nairobi. Kwa maana wale watu wanatafuta important services wanaenda Nairobi and they spend the whole one week wasting the tax payers' money waiting for a very important service.

I propose that the police post be scrapped because it is a source of all evil in our society, promoting corruption and all kinds of evil. Instead of having a police force, we may have a community police whereby those people in charge of the security machineries live with the people, they come from among the people. If we have that kind of a system the corruption we are experiencing from the police will cease because it will be very hard to ask from your neighbour for something small for you to render services.

I also propose that when we have created the States, the local authorities, that is the mayor and the governor be given full mandate to seek for donor funding, for support from outside to develop their local state. You'll ask me what will happen with some provinces like North Eastern Province and Eastern where resources are quite limited. To be able to accommodate that kind of a society, I propose we may take all Industries and all manufacturing companies from Nairobi, relocate these services to those less agricultural productive areas like North Eastern Province and the Eastern Province so that we refer to those states as industrial states and Nairobi is only left to serve as a centre for the finished goods. But the real manufacturing process be done in the less fortunate and unagricultural provinces like the North Eastern Province and the Eastern Province.

I also propose education system be opened up. The tribal problems we have today is as a result of the quota system which was introduced within our government, and which has sort of made the Luhyas to be Luhyas and the Kikuyus to be Kikuyus and the Luos to be Luos. I propose we may scrap up that system and open it up. So that a child who has performed well for example in our constituency like Emuhaya, that child can get a chance in a secondary school even in Eastern Province or in North Eastern province. That will help us to destroy the tribal foundations which have been created by the quota system of education.

I propose also that the 8-4-4 system be scrapped. Of course I know this is not the right forum to address that. The 8-4-4 be scrapped that we may revamp back to our older system whereby we send to the university quite well matured brains to be able to handle the pressure at the university level.

And I propose in our new Constitution we may have a cultural subject. We should put up in school a cultural subject. This cultural subject will be able to intergrate our cultural backgrounds and bring out a real Kenyan cultured kind of being than what we are today because we seem not to know where we really belong.

Briefly, on land matters, I propose that, we may borrow the British system whereby the local authority is given full mandate to control the land. Because in our country we have very big chunks of land not being used because either those people who own them are absent or they have no plan. So the local authority be given the full mandate to cultivate these lands so that they can be productive hence be able to improve the economic stability of the citizens or of the local state Members.

In order to be able to reduce the slum problems, I propose that the Central Government through the Constitution, comes up with a balanced payment scale whereby those who have afforded to be in a full time employment are able to be paid well so that they afford a decent living.

And as I finish, I propose also that the Local authorities be given the full mandate to source for funding and to source for donors so that all the local resources collected, they should be pumped back at the constituency level or at the state level to develop the place. This will help us in one way, that the money we collect for example in Vihiga or in Emuhaya constituency will come back

to us, will lift up the standard of living around this place and we will be able to catch up.

Now, I also Propose that on Chief's act, (I am just finalising) the office of the Chief be retained yes but the powers be reduced. So that the chief becomes a servant of the people. And he should be subjected to election like any other public office. This will help us in reducing the powers which have been abused by the chiefs in using the local administration police as their cover up.

My final proposal, I propose that we may do away with identity cards. Instead, every Kenyan citizen be given a passport and a birth certificate as identification documents thank you.

Com. Ayonga: Bwana Bukachi, asante. Lakini ningependa kukuuliza swali na pengine Commissioners wenzangu wangependa kukuuliza swali. Swali langu ni hili, umesema Police force iwe scrapped and instead form a community police force. A little while ago, somebody said the reason why we have so many crimes in the country is because we have some of the forces who have been disciplined and sent back home, wanachangia crimes kwa maana watu hawa walikuwa wamezoea pesa. Now tunapo-scrap hii police force, hawa maelfu ya Police men and Police Women ambao tunao, baada ya kutolewa kazi huko wanakuja hapa nyumbani. Wengine ni Wanyore wenyewe, wengine ni Wakisii Wanarudi kule kwao nyumbani na inaonekana kwamba wengi wao wanaenda kuchangia crimes, utawapeleka wapi? Uliwafikiria? You don't have to answer me kama ulikuwa haujawafikiria. And tutafanya nini na hao kuwatoa kabisa au tunawarudisha nyumbani waende ku-play the role of community Policemen au wanatolewa na tunaanza na watu wapya at ago.

J . J Bukachi: Kukujibu Bwana Commissioner, we have two options. Option number one. Wale officers ambao their service is commendable, wamefanya kazi mzuri and they are good for the people, tunaweza kuwarudisha for retraining. Kwa maana kile kimetendeka in our society, polisi have been seperated away from the people. They don't live in reality, they live in another lifestyle that is out of the reach of people. That is why when they retire they are not able to continue with that kind of lifestyle. They have got to face reality. Kwa hivyo we bring those whose services have been comendable warudishwe wakuwe retrained on how to live with people. So that they understand that the gun is not the answer. The answer is communication. Some of them can be trained in different aspects. For example counsellors, serious counsellors to handle crime, the kind of people who are always involved in crime, they can be retrained so that now instead of living in the Police camps wanakaa na sisi. They become our neighbours and then they will be retained on a payroll. That would have saved the government pesa nyingi sana ambazo tunatumikia kwa kujenga nyumba za Polisi. Kwa sababu polisi atakuwa anatoka kwake na ni jirani wangu, we have a good relationship, anaenda kutumikia community.

Com. Nunow: Bwana Bukachi, a few clarifications that I would like to seek. One is a follow up of the community policing. You might be aware that Kenya has started training police on community polising now and I think they started with Nairobi and probably going out of Nairobi, so that might be a beginning. You might see how the new skills they acquire on community polising some of whom are already sent abroad in countries where community polising, has taken root to come back and train others, but that is as far as it goes.

On the issue of national schools I mean you mentioned quota system of education being abolished so that students get a chance to go to any other training school they qualified for. That is a noble idea but the distribution of those good schools in itself is acute and they are already located on what is a key to a huge imbalance with some concentration in various areas and none in other areas. So would you stretch the quota system and leave it at that or you would go further and say you know the decentralisation of the good schools, centre, of excellence, so that as you send your kids from here to Mang'u, the Kiambu children are able to come here because there is an equivalent school in Emuhaya or Vihiga.

And the issue of relocating industries to the drier areas, are you suggesting that, that should be done for all industries or you exclude agricultural industries? The reason being the cost of taking those raw materials as bulky as they are across long distances, how would you reconcile that? Because then the cost of production will be increased which then will be passed over to the consumers and then resulting into commercial agricultural products that are expensive and probably difficult for people to acquire.

On the other hand, the so called arid and semi arid areas also might have resources. It is only that probably you have not been able to see them. For instance, 75% of the meat consumed in Kenya comes from Northern Kenya, that is stretch from Samburu up to Lamu, and there have been no industries to address that. You probably would like to think through stock taking, rationalisation, to see indeed what resources exist where, before even assuming that some areas are endowed and others are less endowed. But the key question is, how do you reconcile if you are to relocate agricultural industries, the cost of production shooting up?

J . J Bokachi: Now I don't see the cost of production shooting up because the very very manufactured goods in Nairobi are still bought to the North Eastern Province and so what I am trying to propose here is let's look at the Japanese kind of system whereby you have particular cities known for industrial work and as you may discover that Nairobi is a slum city and in fact we are not proud as Kenyans to have Nairobi as our capital city because it doesn't bring out the image other cities bring out. For example if we took all this manufacturing firms, companies, factories, and we relocate them in Northern Eastern, Eastern province, it means we are going to have a very big exodus from Nairobi to the North Eastern province. What's going to happen now. These people as they come, they are going to promote high level of currency circulation. Now the town or that city or that state which we had thought before that is a very poor State because in this country we heavily depend on Agriculture, and looking at North Eastern province, agriculture cannot work either due to little rainfall and may be the government has not moved in to come up with boreholes so that there is sufficient water.

Now, that problem can be tackled because what will happen when an investor comes here and is taken to the North Eastern and is told, "Now look, this is the place we have available for you because this is our industrial city or industrial State, you've got to develop here." These very very people will begin to deal with one thing to find how to get water and when water is found then

anything can happen. Because everybody who is being relocated there will not find it being a problem. The question of the high cost of consumer goods, what is going to happen is that means and ways will be provided for and I believe when you see a goat is pregnant, when it gives birth you will find things are moving. The problem is we don't think along that area and we think it cannot work. And that is why we have been at stand still. But if there is a mechanism put in place and we all look forward that we want to see this thing move, definitely a way is going to be found. We'll have enough water supply we may not be able to term that province as unagricultural or it might not deal with an agricultural product.

But we can also note some other fertile kind of a province. Take for example Rift Valley, we call it an agricultural state where all kinds of agricultural produce are got from and then we can have at it's extreme far end factories that can deal with all agricultural produce and I believe that every province in this country has some enormous resources that can be used. For example like Emuhaya you can see because all the tourists are taken elsewhere we have dry stones and those people who have read geography, they know that stones are a very good resource for teaching and education and anybody who wants to persue that area, is able to learn so many things around here but what has happened? We cannot have anybody coming because it seems that our resources are concentrated on one place only, as a result of that the rest of the country is dying in languishing poverty.

Com. Ayonga: Thank you very much now you can submit your papers at registration area. Next is Mama Dora Ingolo.

Dora Ingolo: My names are Dora Ingolo. Mimi ni mwenyekiti wa Maendeleo ya Wanawake, Vihiga district na nina memorandum ya Maendeleo ya Wanawake ambayo nitapeana lakini I have also memorandum yangu binafsi ambayo I want to highlight some points.

Katika memorandum yangu I first want to highlight on vulnerable groups in this country. And under vulnerable groups I have identified thirteen vulnerable groups including women, children, veteran, unemployed, the elderly, retirees, touts and drivers, boda boda, disabled, local bar and hotel attendants, HIV aids ophans, widows and widowers. May be I will highlight on a few of them starting with women.

Affirmative action should be put in practice at every level of governance and monitoring should continue to make sure it is implemented.

Civic education to be a continous exercise for both women and men to ensure every one is conversant with the Constitution, in order to ensure everyone's rights are being upheld by those in power at every level.

We need at least 50% of representation of women in every area of decision making to realise women's participation. This should be capable qualified women for indented positions.

Men women and girls and even boys should be treated equally according to their human and basic rights in all places of need, interest, education, culture and employment.

Cultures that are negative on women, like in this District of ours, the Tiriki believe that women cannot be in positions like in the

provincial administration, such cultures should be done away.

Violence against women should be fully addressed by the Constitution and it must provide for a monitoring to ensure the culprits are brought to book and appropriate punishment awarded. This should be done through the Gender Commission, which I recommend should be formed.

During rape case reporting, women police should attend to the victims and should ensure the rapists are brought to book and the right punishment is taken up. Preferably, I recommend such people should be castrated.

Women work hard tirelessly towards the economy of this country but they realise very little benefit from all that they work upon. They should be allowed by the Constitution to reap atleast 50% of their income even at family level.

Children have been mistreated in this country even by the government, parents, employers and even the teachers in school. I therefore recommend the following to be observed in the Constitution;

Every Kenyan to be conversant about the new Childrens Act, which came into use recently. This should be done through provision of civic education.

Children should be given forums at all levels to participate in decision making, because this will reduce the strikes that have become rampant in our institutions, especially in secondary schools.

Primary education and nursery should be free and really free. This must be compulsory to every Kenyan child.

Secondary education should be affordable to all parents. Therefore the Constitution must ensure that fees is controlled to a standard affordable to a local Kenyan.

Abortion should be discouraged and the victim should be punished by the law.

Irresponsible parents who neglect their children should be punished and forced to take care of their children.

The Affiliation Bill, I propose should be revived.

Let me highlight on the youths. For those that have comfortably completed school, they should be taken to colleges, trained and employed by the government of the day.

University education should be made affordable to all Kenyans. All the qualified youths should be admitted without too much strain to the parents. They should be given loans.

Youths who drop out of school should not be left idle but they should be trained in a given skill, and be given loans to start their own busines or be employed.

The use of abusive drugs and selling of the same should be fully addressed in the Constitution.

Recruitment of the youths to trainings should be completely changed. The present mode of recruitment leaves too much room for malpractises where most parents loose large amounts of money in the name of kitu kidogo before their youths are admitted. Hence most of them are not admitted, despite the fact that their parents have paid the amount in question. The girls are exposed to sexual abuse by some people with promises of being employed or given chances in colleges. The people who are found in such deals should be prosecuted and sent to prison.

Now, clubs. Football, music, drama, netball, athletics and so on should be organised from village level to national level to occupy the youth, for competition at all levels identifying their talents and the final stages should be employing them as national

players in different fields according to their talents, like national players in football. This will improve the standard of games or sports in this country.

